**MKUTANO MAALUMU WA WAKUU WA NCHI NA SERIKALI WA AU KUHUSU AJENDA YA CAADP BAADA YA MALABO**
**9-11 JANUARI 2025**
**KAMPALA, UGANDA**

**Ext./Assembly/Decl./3(XIX)**
Lugha chanzi: Kiingereza

# Azimio la Kampala la CAADP kuhusu Kujenga Mifumo Endelevu na Himilivu ya Kilimo na Chakula Barani Afrika

**Sisi**, Wakuu wa Nchi na Serikali za Umoja wa Afrika (AU), tunapokutana kwenye Mkutano wa Kipekee Kampala, Uganda, kuanzia tarehe 9 hadi 11 Januari 2025 tunathibitisha Kudhamiria kwetu kwa Mpango Kamili wa Maendeleo ya Kilimo barani Afrika (CAADP). Tunatambua hitaji la haraka la kufanya upya juhudi zetu za kuendeleza maendeleo ya mifumo thabiti, jumuishi na endelevu ya vyakula na kilimo barani Afrika.

**TUKIKUMBUKA** Lengo la 1, Lengo la 5 la Ajenda ya 2063, ambalo linalenga kuboresha kilimo kwa ajili ya kuongeza uzalishaji.

**TUKIKUMBUKA ZAIDI** Azimio la Malabo la Mpango Kamili wa Maendeleo ya Kilimo wa Afrika (CAADP), lililopitishwa wakati wa Kikao cha Kawaida cha Ishirini na Tatu cha Mkutano wa AU huko Malabo, Guinea ya Ikweta, mnamo Juni 2014, ambapo Nchi Wanachama zilijitolea kufanya mabadiliko ya kilimo jumuishi. Azimio la Malabo CAADP lilithibitisha tena maazimio ya awali, ikiwa ni pamoja na Azimio la Maputo la 2003 kuhusu CAADP na Azimio la Sirte la 2004 kuhusu changamoto za utekelezaji wa maendeleo jumuishi na endelevu katika kilimo na maji barani Afrika.

**TUKITAMBUA** kwamba idadi ya watu barani Afrika inakadiriwa kufikia watu bilioni 2.5 ifikapo mwaka 2050 wakati idadi ya watu ulimwenguni inatarajiwa kufikia watu bilioni 9.8 na kufahamu changamoto ambazo hii italeta kwa mahitaji ya chakula na hitaji la ongezeko kubwa la uzalishaji wa kilimo, usindikaji wa chakula na biashara.

**TUKITAMBUA** athari kubwa za mabadiliko ya tabianchi kwenye kilimo na mifumo ya chakula, hasa kwa watu walio katika mazingira magumu na kusisitiza umuhimu wa majibu ya ubunifu ambayo yanahakikisha upatikanaji wa chakula salama, cha bei nafuu na chenye lishe huku ikiimarisha ushirikiano na ahadi za kimataifa kwa mifumo endelevu.

**TUKIZINGATIA** ukuaji wa haraka wa miji na mabadiliko ya mifumo ya matumizi kuelekea vyakula vilivyo tayari kuliwa na kusindika, tunatambua jukumu muhimu la kuimarisha sekta ya usindikaji wa chakula ili kuunganisha wakulima wadogo na wakulima wengine wowote na kupanua masoko ya ndani na ya kimaeneo. Ingawa inakua kwa kasi, sekta ya usindikaji bado iko katika hatua zake za mwanzo. Afrika, kwa hivyo, ina fursa ya kuunda njia ambayo inakuza teknolojia na mazoea ya usindikaji wa chakula yanayolenga kuongeza matokeo ya lishe.

**TUKITAMBUA** athari ya mabadiliko ya uvumbuzi wa kiteknolojia, maendeleo katika kilimo dijitali, teknolojia ya kibayoteknolojia na kilimo sahihi ili kubadilisha mifumo ya kilimo barani Afrika, pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya simu za mkononi na vifaa vya kidijitali vinavyoimarisha ufikiaji wa wakulima kwa taarifa muhimu, huduma za kifedha na masoko.

**TUKIZINGATIA KWA WASIWASI** changamoto kubwa zinazosababishwa na mabadiliko ya tabianchi, uharibifu wa mazingira na ukosefu wa utulivu kijamii, bara la

Afrika linakabiliwa na masuala tata yanayoathiri uzalishaji wa kilimo moja kwa moja. Mabadiliko ya mitindo ya mvua, kuongezeka kwa joto na mabadiliko hasi ya tabianchi yanaonyesha hitaji muhimu la usimamizi endelevu wa ardhi na maji, pamoja na kilimo kinachozingatia hali ya tabianchi. Kwa kuongezea, kushughulikia ukosefu wa utulivu wa kijamii, hasa uhamiaji unaosababishwa na migogoro, ni muhimu wakati bara linakabiliana na athari za hali ya hewa na upungufu kwenye uzalishaji.

**TUKITAMBUA** jukumu muhimu la masuala ya kijinsia katika kilimo, ni muhimu kuwawezesha wanawake na makundi yaliyo katika mazingira hatarishi kwa sababu wao ni sehemu kubwa ya nguvu kazi ya kilimo katika nchi nyingi za Kiafrika. Ni muhimu kuondoa vizuizi vya kupata rasilimali kama vile ardhi, mikopo na pembejeo za kilimo ili kuongeza uzalishaji kwa kiasi kikubwa na kuboresha usalama wa chakula na lishe. Kwa hivyo, sera na hatua zinazozingatia jinsia ni muhimu katika kubadilisha sekta ya vyakula na kilimo na kujenga jamii zenye nguvu zaidi na Himilivu.

**TUKIANGAZIA** uwezo mkubwa wa ushiriki wa vijana, idadi ya vijana inayokua kwa kasi barani Afrika inatoa fursa ya kuendesha uvumbuzi na maendeleo kwenye kilimo. Tukiwapa vijana mafunzo, ushauri na ufikiaji kwenye rasilimali muhimu, tunawawezesha kuwa mawakala wa mabadiliko katika mifumo ya chakula na kilimo. Ushiriki huu haushughulikii tu masuala makubwa kama ukosefu wa ajira na uhamiaji wa vijijini kuelekea mijini, lakini pia huingiza mitazamo na nishati mpya na kukuza mifumo ya vyakula na kilimo yenye nguvu zaidi na yenye maono kijamii.

**TUKIZINGATIA** kwamba sera za biashara na ujumuishaji wa kikanda, mipango kama vile Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA) ni muhimu katika kubadilisha mifumo ya kilimo na vyakula barani Afrika. AfCFTA ingependa kuimarisha biashara barani Afrika kwa kupunguza ushuru, kuondoa vizuizi vya biashara na kuoanisha viwango, ili kuongeza ufikiaji wa soko na kukuza uhusiano thabiti wa kiuchumi kati ya mataifa ya Afrika. Ujumuishaji huu unaimarisha ushindani kwenye kilimo na uHimilivu na kuliweka bara la Afrika kwenye ukuaji endelevu.

**TUKITAMBUA** jukumu muhimu la ujumuishaji wa viwanda vya kilimo ili kuchochea ukuaji wa uchumi, uundaji wa ajira na ustawi wa pamoja, ni muhimu kuunganisha uzalishaji wa kilimo katika minyororo mipana ya ugavi ili kupambana na ukosefu wa usalama wa chakula na kuboresha lishe. Ili kufikia lengo hili, hata hivyo, tunahitaji uwekezaji kwenye mifumo ya uvumbuzi wa teknolojia, huduma bora, miundombinu, pamoja na sera, udhibiti na mipangilio ya kitaasisi ili kuongeza utendaji na ushindani katika sekta inayoibuka ya usindikaji wa vyakula na kilimo.

**TUKITAMBUA** uwezo wa mabadiliko ya teknolojia zinazoibuka ili kuongeza uzalishaji na uHimilivu kwenye mifumo ya vyakula barani Afrika, ubunifu huu hutoa suluhisho muhimu kwa changamoto kubwa kama vile ukosefu wa usalama wa chakula na lishe na mabadiliko ya tabianchi kwa kuboresha mbinu za kilimo na usimamizi wa rasilimali. Kutumia mitambo, kilimo dijitali, teknolojia ya kibayoteknolojia na maendeleo mengine ya kiteknolojia ni muhimu katika kuongeza ufanisi, uendelevu na usawa kwenye sekta hiyo.

**TUKISISITIZA** kwamba usimamizi endelevu wa maji, hasa katika maeneo yenye uhaba wa maji, ni muhimu katika mabadiliko ya mifumo ya chakula na kilimo barani Afrika. Utekelezaji wa mbinu madhubuti kama vile umwagiliaji kwa kudondosha matone, ukusanyaji wa maji ya mvua na urejelezaji wa maji ni muhimu katika kuongeza uzalishaji wa kilimo katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na ukuaji wa idadi ya watu. Uwekezaji kwenye miundombinu ya maji na matumizi endelevu ya usimamizi ni muhimu katika kuimarisha uHimilivu katika mifumo ya vyakula na kilimo na kuhakikisha uendelevu wake kwa muda mrefu.

**TUKIZINGATIA** mahitaji anuwai ya wakulima, kutoka kwa wakulima wadogo hadi wakubwa, ni muhimu katika kufikia mabadiliko endelevu ya mifumo ya vyakula na kilimo. Wakulima wadogo mara nyingi hupambana na ufikiaji mdogo wa rasilimali, wakati wakulima wa kati na wakubwa wanakabiliwa na vikwazo vya udhibiti na vifaa. Sera na mifumo mahususi ya usaidizi ni muhimu katika kushughulikia changamoto hizi tofauti, kuwawezesha wakulima wote kuongeza uzalishaji, kukuza ukuaji wa usawa na kuimarisha usalama wa chakula na lishe katika bara zima.

**TUKISISITIZA** kwamba mabadiliko kutoka kwa mbinu inayoongozwa na kilimo kwenda kwenye mifumo ya vyakula na kilimo, yatashughulikia changamoto kwenye mfumo mzima wa vyakula na kilimo, wakati wa kuoanisha sera na malengo mapana ya maendeleo. Mbinu hii kamili inaweka kipaumbele kwenye uendelevu wa mazingira, kukuza lishe anuwai yenye kupambana na utapiamlo na kuhakikisha ujumuishaji wa kiuchumi kwenye idadi kubwa ya watu wa kilimo barani Afrika. Ajenda hii pia inalenga kupanua ufikiaji kwenye soko na kukuza biashara ya kikanda, hasa kupitia Eneo Huru la Biashara la Bara la Afrika (AfCFTA), kwa lengo la kuongeza kwa kiasi kikubwa biashara ya kilimo ya ndani ya Afrika.

**TUKITAMBUA** umuhimu wa kupunguza hasara baada ya mavuno, tunasisitiza hitaji la kukuza ubunifu katika utunzaji, uhifadhi na usafirishaji baada ya mavuno ili kupunguza hasara ya chakula na kuboresha upatikanaji wa chakula na mapato kwa wakulima.

**TUKIKARIBISHA** maazimio ya Kikao Maalumu cha Kamati Maalumu ya Kitaalamu ya Kilimo, Maendeleo ya Vijijini, Maji na Mazingira, kilichofanyika Addis Ababa, Ethiopia kuanzia tarehe 23-25 Oktoba 2024.

**Sisi**, hivyo, tunapitisha ***Mkakati na Mpango wa Utekelezaji wa CAADP: 2026 hadi 2035*** na Azimio lifuatalo la ***Kampala CAADP kuhusu Kujenga Mifumo ya Vyakula Himilivu na Endelevu barani Afrika***

## I. Kudhamiria Kuimarisha Uzalishaji wa Chakula Endelevu, Viwanda vya Kilimo na Biashara

Tunadhamiria kuongeza uzalishaji wa vyakula vya kilimo kwa asilimia 45 ifikapo mwishoni mwa mwaka 2035 kupitia kupitishwa kwa mazoea endelevu ya kilimo ili kukidhi mahitaji ya chakula ya Afrika yanayokua na fursa za biashara ya kimataifa, kupunguza upotevu wa baada ya mavuno kwa asilimia 50, kuongeza mara tatu

biashara ya ndani ya Afrika katika bidhaa na pembejeo za vyakula vya kilimo ifikapo mwaka 2035 sambamba na AfCFTA na kuongeza sehemu ya chakula kilichosindikwa nchini hadi asilimia 35 ya Pato la Taifa la vyakula vya kilimo ifikapo mwaka 2035. Ili kufanikisha hili, tunaazimia:

a) Kuimarisha na kuhakikisha utendaji wa mifumo ya pembejeo za kilimo—ikiwa ni pamoja na mifumo ya mbegu, mbolea, usimamizi wa maji na utafiti wa kilimo na huduma za ugani, huku tukikuza ueneaji wa mbinu endelevu za kilimo ambazo huhifadhi rasilimali, kulinda mazingira na kuhakikisha uzalishaji wa muda mrefu.

b) Kuunda sera endelevu na mazingira ya udhibiti inayokuza maendeleo na ujumuishaji wa teknolojia zinazoibuka, kama vile bayoteknolojia, akiliunde, kilimo dijitali na sahihi.

c) Kuhamasisha ukuaji, ushindani na uendelevu wa biashara za kilimo na viwanda, kwa kuzingatia hasa biashara ndogo na za kati (SMEs).

d) Kuimarisha ujumuishaji wa wakulima wadogo, wanawake na vijana kwenye minyororo ya thamani na masoko ya kikanda, huku wakiendeleza na kuimarisha minyororo hii ili kuchochea ongezeko la thamani katika hatua zote na kuhakikisha ushiriki na faida sawa katika uzalishaji na biashara ya kilimo, wakati wote wakihakikisha kufuata viwango endelevu vinavyokidhi mahitaji ya mazingira na kijamii ili kuongeza ukuaji wa uchumi na ufanisi.

e) Kuimarisha upatikanaji wa soko na uwezeshaji wa biashara kwa kuondoa vikwazo vya biashara na kuboresha miundombinu kwa ajili ya usafirishaji bora wa bidhaa.

f) Wekeza katika minyororo ya thamani ya kikanda, miundombinu ya baada ya mavuno, vikapu vya chakula na korido za biashara, kuongeza ushirikiano wa kikanda, kuongeza biashara ili kuboresha usalama wa chakula na lishe katika Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika.

## II. Kudhamiria Kuongeza Uwekezaji na Ufadhili kuharakisha Mabadiliko ya Mifumo ya Chakula na Kilimo

Tunadhamiria kuhamasisha jumla ya dola bilioni 100 katika uwekezaji wa umma na binafsi katika mifumo ya vyakula vya Kiafrika ifikapo mwaka 2035, huku tukihakikisha kuwa angalau asilimia 10 ya matumizi ya kila mwaka ya umma yanatengwa kwa mifumo ya vyakula vya kilimo na kwamba angalau asilimia 15 ya Pato la Taifa la vyakula vya kilimo huwekezwa tena kila mwaka katika sekta hiyo. Ili kufikia lengo hili, tunaazimia:

a) Kuongeza uwekezaji kwenye sekta ya umma na binafsi katika mifumo ya vyakula na kilimo ili kuchochea ukuaji endelevu na uvumbuzi.

b) Kupanua uwekezaji kwenye sekta ya umma ili kusaidia miundombinu na mipango muhimu ndani ya mifumo ya chakula na kilimo.

c) Kuimarisha uwezo wa kuendeleza na kutekeleza mipango muhimu na miradi inayoweza kufikiwa na benki, kuhakikisha kuwa uwekezaji unasababisha matokeo athirifu na yanayoweza kufikiwa.

d) Kuboresha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mabadiliko ya mifumo ya kilimo na chakula, kuwezesha ushiriki mkubwa kutoka kwa wadau katika sekta zote, kuhakikisha hasa kwamba viwango vya kutosha vya fedha zinazotolewa kwa matunzio ya hali ya hewa huwafikia wakulima na wazalishaji, wasindikaji wadogo wa chakula na wale wa kati.

**III. Kudhamiria Kuhakikisha Usalama wa Chakula na Lishe**

Tunadhamiria kufanikisha kutokuwa na njaa katika Nchi zote za Umoja wa Afrika ifikapo mwaka 2035 na kupunguza kudumaa kwa asilimia 25, kupoteza kwa asilimia 25 na uzito kupita kiasi kwa asilimia 25, kuhakikisha kuwa asilimia 60 ya idadi ya watu wanaweza kumudu lishe bora. Ili kufikia lengo hili, tunaazimia:

a) Kukuza mifumo ya vyakula na kilimo inayoimarisha lishe ya binadamu na matokeo ya afya, kukuza lishe zinazochangia ustawi kwa ujumla.

b) Kukuza uzalishaji na matumizi ya mazao ya kiasilia yenye lishe, wanyama, samaki na mazao ya uvuvi kupitia mageuzi mahususi ya sera na udhibiti na mikakati ya ufadhili kwa minyororo hiyo ya thamani.

c) Kuimarisha sera za lishe, mipango, elimu na uelewa wa watumiaji ili kuondoa upungufu wa virutubisho vidogo.

d) Kuongeza viwango vya Usafi na Viwango vya Saikolojia na Afya (SPS) na kutekeleza itifaki za Afya Moja ili kudumisha usalama wa chakula na kulinda afya ya binadamu, wanyama, mimea na mazingira.

e) Kuwekeza katika ufuatiliaji wa magonjwa na kuripoti, kuimarisha maabara za mifugo, kuongeza uzalishaji wa chanjo, kuweka kipaumbele katika kutokomeza wadudu wadogo wa weusi waharibifu wa mazao (PPR) ifikapo mwaka 2030 na kuboresha ushirikiano katika magonjwa ya wanyama yanayovuka mipaka.

f) Kutanguliza utafiti na maendeleo ya aina bora za mazao ya lishe na kukuza vyanzo mbadala vya malisho ili kuongeza lishe ya mifugo na kupunguza utegemezi wa malisho ya jadi.

g) Kuimarisha minyororo ya thamani ya uvuvi na ufugaji wa samaki wakati wa kukuza mazoea endelevu, kujenga uHimilivu na usimamizi mzuri na endelevu wa rasilimali za majini.

h) Kuendeleza ubunifu mkubwa wa kiusalama na kijamii unaoshughulikia utapiamlo kwa ufanisi na kukuza usalama wa chakula na lishe.

## IV. Kudhamiria Kuendeleza Ujumuishaji na Shughuli za kujiingizia kipato Zenye Usawa

Tunadhamiria kupunguza idadi ya watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri kwa asilimia 50, kupunguza pengo la mavuno kati ya wakulima wanaume na wanawake kwa asilimia 50 na kuwezesha angalau asilimia 30 ya wanawake na makundi yaliyo katika mazingira hatarishi, asilimia 30 ya vijana na asilimia 30 vikundi vilivyotengwa katika minyororo ya thamani ya vyakula ifikapo mwaka 2035. Ili kufanikisha hili, tunaazimia:

a) Kuboresha miundombinu na upatikanaji wa huduma za kijamii katika maeneo ya vijijini na jamii zilizo katika mazingira hatarishi.

b) Kupunguza pengo la mavuno kati ya wakulima wa kiume na wa kike.

c) Kuwezesha ufikiaji wa rasilimali zenye tija ikiwa ni pamoja na huduma nzuri za kifedha, uvumbuzi, teknolojia na ufikiaji wa ardhi kwa wanawake, vijana na makundi yaliyo katika mazingira hatarishi.

d) Kuwezesha ajira za hali ya tabianchi na za kijani kwa vijana, wanawake na vikundi vilivyotengwa kupitia mipango inayosaidia biashara zinazozingatia kilimo bora cha hali ya tabianchi, nishati mbadala katika biashara ya kilimo, masoko ya kaboni na kukabiliana na hali ya hewa.

e) Kutekeleza mipango jumuishi ya kulinda jamii inayoshughulikia mahitaji ya watu walio katika mazingira magumu.

## V. Kudhamiria Kujenga Mifumo Himilivu ya Chakula

Tunadhamiria kuhakikisha kuwa mifumo ya vyakula vya kilimo barani Afrika inastahimili majanga ya hali ya hewa, kijamii na kiuchumi na mazingira. Tunaahidi kuwa na angalau asilimia 30 ya ardhi ya kilimo chini ya usimamizi endelevu na asilimia 40 ya kaya zinazolindwa kutokana na majanga ifikapo mwaka 2035. Ili kufanikisha hili, tunaazimia:

a) Kuongeza uwekezaji katika uwezo wa kibinadamu na kimwili kwa ajili ya utafiti ili kuzalisha teknolojia za kilimo na ubunifu unaopunguza mabadiliko ya tabianchi.

b) Kuimarisha mifumo ya onyo na mwitikio wa mapema kwa mshtuko anuwai wakati wa kutekeleza mikakati ya kitaifa ya uHimilivu ambayo inajumuisha uHimilivu katika mipango na sera, mwishowe kuhamasisha rasilimali kwa ajili ya kujenga uwezo katika mifumo ya chakula na kilimo.

c) Kuongeza uwezo wa kufyonza wa mifumo ya vyakula na kilimo ili kupunguza uharibifu, kulinda maisha na kusaidia juhudi za kuimarisha kufuatia mshtuko au usumbufu.

d) Kukuza mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ndani ya mifumo ya chakula na kilimo na maisha ili kupunguza hatari ya majanga makubwa na mafadhaiko.

e) Kuongeza uhamasishaji kwa ufadhili wa hali ya hewa na msaada wa kiufundi kusaidia wakulima, hasa wakulima wadogo na mabadiliko kwenye matumizi ya kilimo cha kaboni ya chini.

f) Kukuza maarifa na mazoea ya asili, kutambua jukumu lao katika kukuza uhifadhi wa mazingira na uHimilivu.

**VI. Kudhamiria Kuimarisha Utawala wa Mifumo ya Chakula na Kilimo**

Tunadhamiria kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka wa 2028, Nchi zote Wanachama wa Umoja wa Afrika na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda (REC) zinaunganisha Azimio la Kampala CAADP katika mipango yao ya kitaifa na kikanda ya uwekezaji wa mifumo ya chakula cha kilimo na kupitisha mazoea bora katika utawala wa mifumo ya chakula cha kilimo kulingana na kanuni za CAADP. Zaidi ya hayo, ifikapo mwaka wa 2030, nchi zote zitajumuisha mchakato wa Mapitio ya Biennial ya CAADP katika majukwaa yao ya kitaifa ya mapitio ya pamoja ya sekta ya kilimo. Ili kufanikisha hili, tunaazimia:

a) Kudumisha kanuni za CAADP ambazo ni pamoja na ukuaji wa uchumi unaoongozwa na chakula kwa ajili ya maendeleo jumuishi na endelevu; ukamilishaji wa kikanda na ushirikiano; na ushiriki jumuishi wa wadau wote, hasa wanawake, vijana na makundi yaliyo katika mazingira hatarishi.

b) Kukuza uamuzi unaotegemea ushahidi na uwajibikaji wa pande zote, kuhakikisha kuwa vitendo vinaongozwa na data ya kuaminika.

c) Kuimarisha Tume ya Umoja wa Afrika, AUDA-NEPAD na REC ili kuwawezesha kutimiza majukumu na mamlaka yaliyoainishwa kwenye azimio hili.

d) Kuandaa chombo cha kifedha kilichoundwa kusaidia utekelezaji mzuri wa Azimio hili.

e) Kuwezesha mabunge ya kitaifa, kikanda na mabara na kamati zake, ili kuhakikisha uoanishaji thabiti wa sheria na bajeti za kitaifa na malengo ya Azimio la CAADP la Kampala, na kuweka usimamizi kwa ajili ya utekelezaji bora wa sera husika.

f) Kuimarisha mashirika ya wazalishaji ili kuwawezesha kutimiza jukumu lao katika kuendeleza na kutekeleza sera za kitaifa na kikanda, pamoja na mamlaka yaliyoainishwa katika Azimio hili.

**VII. Wito wa Kuchukua Hatua**

Sisi, Wakuu wa Nchi na Serikali tunatambua kwamba ili kufikia malengo na maazimio yaliyoainishwa katika azimio hili itahitaji uhamasishaji wa wadau wengi ili kubadilisha maamuzi haya kuwa matokeo dhahiri. Ili kufanikisha hili, tunatoa wito kwa:

a) **Nchi Wanachama**:

- Zijumuishe na kuonyesha ahadi kwenye azimio hili katika sera za kitaifa, mikakati na mifumo ya bajeti, kwa utekelezaji mzuri kupitia Mipango ya Taifa ya Uwekezaji wa Mifumo ya Kilimo (NASIP) na kuhakikisha kuwa mipango na vifaa bora vya utekelezaji vimewekwa ili kuimarisha NASIP.
- Ziandae na kutekeleza sera kamili, thabiti zinazokuza uwekezaji kwenye sekta binafsi katika mabadiliko ya mifumo ya chakula wakati wa kuhakikisha msaada mzuri kwenye sekta ya umma katika mifumo hii.
- Ziongeze uwekezaji kwenye miundombinu, utafiti na huduma za ugani ili kusaidia kuharakisha mabadiliko kwenye mifumo ya chakula na kilimo.
- Zihakikishe mifumo ya uratibu yenye ufanisi ipo na kuna ushiriki jumuishi katika utawala wa mifumo ya vyakula na kilimo kwa umakini maalum kwa wanawake, vijana na makundi yaliyo katika mazingira hatarishi.
- Zihakikishe uwezo wa kutosha na kuteua timu ya ufuatiliaji na tathmini ya apex, inayoungwa mkono na mifumo ya maarifa ya Afrika nzima, wataalam wa kiufundi na majukwaa madhubuti ya kidijitali ya kupima ufanisi wa utendaji na usimamizi wa data.

b) **Umoja wa Afrika (AUC na AUDA-NEPAD) na Jumuiya za Kiuchumi za Kanda (RECs)**:

- Kusaidia Nchi Wanachama wa AU na REC kuweka ahadi katika azimio hili katika Mipango ya Uwekezaji ya Mifumo ya Kilimo ya Kitaifa na Kikanda (NASIP na RASIP).
- Ziwezeshe ushirikiano wa kikanda, ujumuishaji wa kiuchumi na uoanishaji wa sera katika nchi za Wanachama wa Umoja wa Afrika ili kukuza biashara ndani ya Afrika.
- Zianzishe baraza la ushauri linaloongozwa na sekta binafsi ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi.
- Zifanye Mchakato wa Ukaguzi wa Kilimo wa miaka miwili, kuanzia mwaka wa 2027 na kuripoti maendeleo kwenye Bunge wakati wa Kikao chake cha Kawaida cha Januari au Februari kitakachoanza mwaka wa 2028.
- Ziongeze matumizi ya matokeo ya ripoti ya mapitio ya CAADP ya kila mwaka ili kuarifu upangaji na kufanya maamuzi katika ngazi za kitaifa, kikanda na bara.

e) **Wakulima na wazalishaji wa vijijini** :

- Wapitishe mazoea ya kiubunifu na teknolojia zinazoibuka ili kuongeza uzalishaji kwenye kilimo, uendelevu na uHimilivu.
- Wawekeze katika kuongeza ubunifu kwenye uzalishaji na gharama za ushindani ili kudhibiti sehemu kubwa ya masoko ya ndani na ya kikanda.

f) **Asasi za kiraia** :

- Kutayarisha mfumo mahususi wa kusimamia Mipango ya Uwekezaji ya Mifumo ya Kilimo ya Kitaifa na Kikanda (NASIP/RASIP), kuhakikisha uwazi na uwajibikaji katika utekelezaji wake.
- Kuhamasisha ugawaji wa rasilimali kwa ajili ya maendeleo ya mifumo ya chakula cha kilimo, kuimarisha fursa za ufadhili na msaada kwa mipango ya NASIP/RASIP.
- Kuhamasisha mbinu endelevu na zenye usawa za kilimo katika mabadiliko ya mifumo ya chakula na kilimo.

g) **Sekta binafsi** :

- Kuwekeza katika teknolojia, ubunifu maendeleo ya soko na ujumuishaji kwenye mnyororo wa thamani ili kuendesha mabadiliko ya mifumo ya vyakula na kilimo.
- Kuongeza uwekezaji katika minyororo endelevu ya thamani ya vyakula na kilimo ili kuongeza uzalishaji wa chakula, viwanda vya kilimo na biashara.

e) **Wabunge** :

- Kusaidia Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika na RECs katika utungaji na utekelezaji wa sera za Mfumo wa kilimo cha mazao ya chakula na mipango ya uwekezaji katika ngazi za kitaifa na kikanda, kupitia sheria zinazofaa, mgao wa bajeti na uangalizi wa kitaasisi.
- Kuhakikisha kwamba angalau 10% ya matumizi ya kila mwaka ya umma yanawekezwa katika mifumo ya kilimo cha mazao ya chakula na kufuatilia matumizi yake kwa ufanisi katika ngazi za kitaifa na kikanda.

h) **Wabia wa maendeleo na mashirika ya kimataifa**:

- Kujitolea kusaidia utekelezaji wa Mkakati na Mpango wa Utekelezaji wa CAADP: 2026 hadi 2035 na Azimio la Kampala CAADP kwa kuunganisha rasilimali zao za kiufundi na kifedha kwenye vipaumbele vya bara.
- Kusaidia AUC, AUDA-NEPAD na jumuiya za kiuchumi za kikanda kutoa msaada unaohitajika kwa Nchi Wanachama kujumuisha azimio la Kampala CAADP kwenye NAIP au RASIP.
- Kuimarisha mifumo ya data na juhudi za uwajibikaji wa pande zote katika ngazi za bara, kikanda na kitaifa.

Azimio hili litaanza kutumika tarehe 1 Januari 2026

**Limeandaliwa tarehe 11 Januari, 2025 Kampala, Uganda**